KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 21, Issue 4

6th Jumadal-Akhirah 1433

27th April, 2012

TAFSIRI YA QASWIDA YA BURDAI

Na: Shaykh Muhammad Jameel Zeeno (d. 1383 AH / n/a CE)

Kila sifa njema ni zenye kumthubutukia Allaah, Aliyemleta Mtume wake akiwa juu ya uongofu na Dini ya Haki, ili aitwalishe juu ya Dini zote. Allaah anatosha kuwa ni Shahidi wa hayo yote. Yaa Allaah, mfikilizie swala na salamu Muhammad, kama ambavyo ulivyomswalia na kumsifu Ibraahim na wafuasi wa Ibraahim. Kwa hakika Wewe ni Mwingi wa Himdi na Shukrani. Yaa Allaah mbariki Muhammad na jamii ya Muhammad, kama ambavyo ulivyombariki Ibraahim na Jamii ya Ibraahim. Kwa hakika Wewe ni Mwingi wa Himdi na Shukrani.

Ama baada ya hayo: Nilipokuwa katika likizo yangu ya masiku ya joto katika Nchi ya Uingereza, nilipata kuiona "Qaswida ya Burdai" iliyotungwa na Busairi, ikisambazwa na ma-Sufi kama kipimo cha mapenzi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Jambo la kushangaza ni kwamba watu wa kawaida na wanafunzi wamekuwa ni vinyan'ganyiro vya ma-Sufi, wenye kuitumia Qaswida kwa njia ya udanganyifi kama chombo cha kuwalingania watu kwenye imani zao za ufisadi, wakiwavutia waathiriwa wao kwenye imani za ki-Sufi; na kutumia mwito wao mpotofu kwa madai ya kumpenda Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kwa hakika, ma-Sufi huwashawishi walioghafilika kufanya mambo ya uzushi (Bid'ah) na ushirikina Mkubwa [Ash-Shirkul-Al-Akbar].

Mtunzi wa Qaswida hii yenye uvumi mbaya, al-Busairi alimfanya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa ni muombezi wake kwa Allaah, kwa kumuomba yeye (صلى الله عليه وسلم) amsaidie, na ampe utulivu, jambo ambalo Allaah (سبحانه وتعالى) amelieleza kuwa huko ni kumuabudu asiyekuwa Yeye. **"Nao wanaabudu (waungu) - wasiokuwa Allaah - wasioweza kuwadhuru (wanapoacha kuwaabudu) wala kuwanufaisha (wakiwaabudu). Na wanasema: "Hao (waungu wadogo washirika wake tunaowaabudu) ndio waombezi wetu mbele ya Allaah." Sema: "Jee! Mnamwambia Allaah asiyoyajua katika Mbingu wala katika Ardhi?" (Nayo ni kuwa ana washirika. Hayajui haya Allaah mwenyewe). Ameepukana na upungufu (wa kutaka mshirika), na ametukuka na hao wanaowashirikisha nae.** (Surah Yunus Ayah no: 18).

Kupinduka mipaka kwa Busairi na kutofahamu kwake 'ilmu ya Tawheed al-Uloohiyyah kulimfanya afuate nyayo za Mayahudi na Manaswara kuhusiana na ambaye Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyetutahadharisha aliposema: *"Enyi watu! Jitahadharini na kupinduka mipaka (Ghuloow) katika Dini, kwani kwa hakika yale yaliyowaangamiza na kuwahasiri waliokuwa kabla yenu ni kupinduka mipaka katika Dini."*

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Mutafuata njia za waliowatangulia nyinyi, shubiri kwa shubiri na pima kwa pima; kiasi cha kwamba lau wataingia kwenye shimo la mburu-kenge nanyi pia mutawafuata humo."*

Na alipoulizwa iwapo alimaanisha kuwa tutawafuata Mayahudi na Manaswara, alijibu: *"Basi ni nani tena kama si hao?"*

Jambo la kustaajabisha ni kwamba wengi wa wale walioshikilia Qaswida hii ya Burdai kwa "magego" yao, ni wale wenye kudai kuwa ni wafuasi vipofu wa Imaam Abu Haneefah, wenye kujinasibisha na madhehebu ya Deobandee na Barailwee. Ingawaje, Imaam Abu Haneefah alisema: "Haifai kwa mtu yoyote kumuomba Allaah, isipokuwa kama alivyotufunza Yeye Mwenyewe, na kwa maombi aliyoturuhusu nayo na kutuamrisha. Haya yamefahamika kutokamana na matamshi Yake: "**Na Allaah ana majina mazuri, muombeni kwayo. Na waacheni wale wanaoharibu utakatifu wa majina yake. Karibuni hivi watalipwa yale waliyokuwa wakiyatenda.** (Surah Al-A'raaf Ayah no: 180)

Vilevile Imaam amesema: Ni Makuruhu kwa mwenye kuomba kusema, 'Mimi nakuomba kwa haki ya Fulani na Fulani, 'au kwa haki ya

TANGAZO LA MUHADHARA

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA WANAWAALIKA MUHADHARA WA KI-'ILIMU KATIKA MASJID MAZRUI TAREHE 1st MAY, 2012

MAUDHUI NA MUHADHIRI:

ITIKADI YA AHLUS-SUNNAH WAL JAMAA'AH
[USAWA NA UADILIFU]
***USTADH SHARIFF**

HASAD NA ATHARI ZAKE KATIKA MUJTAMA'
***USTADH ISMAA'IL**

WAKATI WA MUHADHARA

KUANZIA BA'DAL ASR MPAKA ISHAA'. 4:15pm - 'ISHAA'
WANAUME WATAKUWA NDANI YA UKUMBI WA MSIKITI NA WANAWAKE WATAKUWA KATIKA UKUMBI WA JUU [WANAPOSWALI].

YALIYOMO

TAFSIRI YA BURDAI	1 - 4
MAZISHI	4
TANGAZO LA DARSA	1

Mitume Yako na Manabii, au kwa haki ya Nyumba Tukufu na mipaka mitakatifu."

Hawa ma-Deobandi na ma-Barailwi wataweza kumbandika majina Imaam Abu Haneefah kuwa ni mpotofu kwa kutomsifu Mtume (صلى الله عليه وسلم) kupita kiyasi kama alivyofanya Busairi? Ikiwa mwenye kujiepusha kumfuata ki-Upofu (taqleed) Imaam Abu Haneefah huzingatiwa kuwa ni mpotofu, aliyepotezwa na kuwa ni mwenye kufuata hawaa za nafsi yake, basi ma-Deobandi na ma-Barailwi ndiwo watakaokuwa wamefanya makosa hayo mbali na kupindukia mipaka kwa jina la Mapenzi, na kumfanya Busairi - ambae hata si msomi wala mwanachuoni, kuwa ni bora - kuliko Imaam wao Abu Haneefah.

Huwenda watu wengi wakagutuka wakisikiya yakwamba muanzilishi wa Jamaa'at ut-Tableegh, Maulana Muhammad Ilyaas alisema kwenye naswaha yake ya mwisho kwa Maulana Yusuf ambae ni mrathi wake:

"Wanavyuoni watatakiwa waisome Qaswida ya Burdai na Shiyamul-Habeeb kwa heshima na unyenyekevu, au kinyume chake bila ya kuiheshimu na kuitegemea haitokuwa na maana yoyote. Kutoka katika kifungu cha … Mafungamano baina ya Qaswida ya Burdai na Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni jambo lilothubutu.

Mimi nasema, mbali na kuwa mtu mwenye kuthibitisha mafungamano na Mtume (صلى الله عليه وسلم), hapo atakuwa yeye mume/mke kwa hakika amezua mafungamano na Ushirikina na wala hatokuwa akimpa daraja isipokuwa muanzilishi wa Jamaa'atut-Tableegh. Malengo yaliyofichwa ya Jamaa'atut-Tableegh yamebainika kwa Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah, ambayo si jengine isipokuwa ni kuhuisha Usufi, kuwaepusha watu wasiokuwa na hatia na kufuata Sunnah, na kuwaongoza kunako mafunzo ya "Sufi mkubwa", Maulana Ilyaas; muanzilishi wake na mwenye kuuhuisha Usufi kwa kupitia kwenye pote lake la Jamaa'atut-Tableegh lenye kukaidi itikadi swaheeh. Ukweli wa mambo ni kwamba, Jamaa'atut-Tableegh wanahuisha na kulingania Da'wah ya ma-Sufi, hata mpaka kwenye vitanda vyao vya mauti. Kwa kumalizia, Enyi Waislamu! Mimi nimeamua kutekeleza uwajibikaji wangu, nikitarajia malipo kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى), Peke yake kwa kuyafasiri kwa lugha ya Kiswahili, mukhtaswari wa Qaswida hii uliotayarishwa na Sheikh Muhammad Jameel Zeeno wa Syria ili ukweli wa Qaswida hii ufichuke kwa Waislamu wa kawaida wasio na hatia. [Sheikh Muhammad Jameel Zeeno (حفظه الله) mwenyewe hapo awali alikuwa ni Sufi kabla ya kuongozwa na Allaah (سبحانه وتعالى), na kuwa kwenye haki].

Kazi hii Insha-Allaah, ni kwa faida ya wale wenye kutafuta ukweli kwa uaminifu pasi na kuwa na upendeleo wala chuki kwa njia yoyote. Ni kwa wale wenye raghba (moyo) ya kumpenda Mtume (صلى الله عليه وسلم), kulingana na walivyompenda Maswahaba zake watukufu, bila ya kutia chembechembe za nyongeza. Twamuomba Allaah atuongoze sote kwenye haki! Ameen!

Hatimae namalizia utangulizi wangu huu kwa maneno makubwa ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): Imepokewa kutoka kwa Anas bin Maalik yakwamba mtu mmoja alimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Ewe Muhammad! Ewe uliye bora miongoni mwetu, na mwanae aliyekuwa mbora miongoni mwetu, kiongozi wetu, na mwanae kiongozi wetu …"

Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu kwa kumwambia: *"Enyi watu! Semeni yaliyo kulingana na mafunzo ya watu walio kwenye imani yenu na Dini yenu; na muniite mimi Mtume na wala musimuache Shetwani awazidi nguvu na kuwashinda nyote kwa kuwafanya muwe ni wawakilishi na wafuasi wake,"* na kisha akasema mojawapo ya mambo mawili: *"Mimi ni Muhammad, mwanae Abdullaah, au mimi ni Muhammad, mja wa Allaah na Mtume Wake, mimi siwataki nyinyi muniinue juu kuliko daraja niliyopewa [iliyotoka] kwa Allaah (سبحانه وتعالى).*

===

Kila sifa njema ni yenye kumthubutukia Allaah, Rabb wa wana-adamu wote, Majini, na kila kitu kilicho katika ulimwengu huu, na twaomba swala na salamu kutoka kwa Allaah zimshukie Mtume Wake muaminifu (صلى الله عليه وسلم), ahli yake pamoja na Maswahaba zake wote. Mwanzo kabisa: …

Shairi hili lililotungwa na Busairi ni maarufu sana miongoni mwa watu, haswa ma-Sufi. Lau kama tungezingatia na kutafakari maana zake, basi kwa hakika tungefahamu na kutambua yakuwa ndani yake mulikuwa na uhalifu na uvunjaji dhidi ya "Qur'an Takatifu na Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم)!"

Amesema Busairi kwenye Mlango wa 10 wa Mashairi yake:

يا أكرم الخلق ما لي من ألوذ به * * *

سواك عند حلول الحادث العمم

Ewe mbora wa viumbe, mimi sina wa kumkimbilia; isipokuwa wewe pindi yakienea maafa.

Mshairi Busairi alikuwa akiomba na kutafuta msaada kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na alikuwa akimwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Mimi siwezi kupata mtu wa kumkimbilia na kutafuta hifadha kwake wakati wa maafa na misukosuko isipokuwa wewe tu.'

Jambo hili limeorodheshwa kuwa ni miongoni mwa Shirk kubwa [ash-Shirkul-Akbar], inayomfanya mwenye kuifanya Shirk hiyo abakie na kuingizwa kwenye Moto wa Jahannam milele iwapo hatotubia kutokamana na kitendo hicho; kwahiyo maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na (nikaambiwa): 'Wala usiwaabudu badala ya Allaah wale ambao hawakufai (unapowaabudu) wala hawakudhuru (unapowaacha kuwaabudu). Basi ukifanya utakuwa miongoni mwa Dhâlimûn (wa nafsi zao)."** (Surah Yunus: Ayah no: 106)

Maana ya neno Dhwaalimun ni: Washirikina na wanaofanya maovu kwa sababu kumuwekea Allaah washirika kwenye 'Ibaada ni Dhulma kubwa: makosa.

Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Yoyote atakaekufa haliyakuwa anawaomba wengine pamoja na Allaah, hapana shaka ataingia Motoni."*

فإن من جودك الدنيا وضرتها

Kwa hakika miongoni mwa ulivyotukarimu nayo ni huu ulimwengu, na akhera.

Huku ni kuikanusha Qur'an ambayo inathibitisha:

'Na ni Yetu sisi Akhera na dunia." (Surah Al-Lail Ayah no.13).

Kwahivyo Ulimwengu huu na Akhera vyote hivyo ni vya Allaah na ni miongoni mwa viumbe Vyake. Therefore this world and the hereafter are both from Allâh and from amongst His creation. Si miongoni mwa ukarimu wala utoaji wa Mtume (صلى الله عليه وسلم), na wala si kwamba ati yeye (صلى الله عليه وسلم) ndiye aliyewaumba hata wawe ni miongoni mwa viumbe vyake.

ومن علومك علم اللوح والقلم

Na sehemu ya 'ilmu yako ni 'ilmu ya kurasa zilizohifadhiwa (Lawh) na kalamu.

Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwa akijua kila jambo ambalo ni katika sehemu ya kurasa zilizohifadhiwa, kwa sababu

hakuna mwenye ‘ilmu yake isipokuwa Allaah Peke yake. Kwa kweli huku ni kusifu kupita kiasi na kutia chumvi kulikoelekezwa kwake Mtume (صلى الله عليه وسلم) maadamu twaeleza na kuamini yakwamba ulimwengu huu na akhera ni miongoni mwa ukarimu na fadhla za Mtume (صلى الله عليه وسلم) Zaidi ya hayo, mashairi yenyewe yameeleza yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) anaijua ‘ilmu ya yaliyofichamana iliyomo katika kurasa zilizohifadhiwa, na kwamba kila kitu kilicho kwenye kurasa hizo zilizohifadhiwa ni miongoni mwa ‘ilmu za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kutia chumvi huku kumekemewa vikali na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akatukataza kupita mipaka katika kumsifu yeye, kama alivyosema yeye (صلى الله عليه وسلم): *“Musinisifu mimi kupita kiasi kama walivyofanya Manaswara kwa ‘Issa mwana wa Maryam; Mimi ni mtumwa tu, kwahiyo badala yake niiteni Mtumwa wa Allaah na Mtume Wake.”*

Vilevile Busairi ameandika kwenye Mlango wa 5 yafuatayo:

◊ **ما سامني الدهر ضيماً واستجرت به * * * إلا ونلت جواراً منه لم يُضَم**

Kila wakati ukinitia dhiki basi mimi hutafuta hifadha kwake. Mimi hupata msaada ambao usiotumika vibaya kutoka kwake.

Asema Busairi: Maradhi yoyote na dhiki zinazonikumba mimi, mimi huelekeza maombi yangu kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa pozo na matibabu. Kwahiyo, kwa nafuu ya dhiki zangu hapana isipokuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ndiye mwenye kunipoza na kunipa afuweni.’ Haliyakuwa Allaah (سبحانه وتعالى) katika Qur’an amesimulia kutoka kwa Ibraahim (عليه السلام) maneno yake: **“Na ninapouguwa, Yeye ndiye anayeniponesha.’** (Surah Ash-Shu’ara Ayah 80).
Allaah (سبحانه وتعالى) akasema: **‘Na kama Allaah akikugusisha madhara (taabu), basi hakuna yoyote awezaye kuyaondoa ila Yeye.’** (Surah Al-An’am Ayah 17)
Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *“Unapo omba, basi muombe Allaah, na unapotaka msaada, taka msaada kutoka kwa Allaah.’*

Katika Mlango wa 9, ameandika:

فإن لي منه ذمة بتسميتي محمداً * * * وهو أوفى الخلق بالذمم

Kwa hakika mimi niko chini ya dhima yake kutokana na jina langu. (Kuwa kwangu ni) Muhammad, akiwa yeye ni mbora miongoni mwa viumbe waaminifu katika kutekeleza ahadi yake.

Asema Busairi: “Kwa hakika mimi nina ahadi kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba ataniingiza Peponi, kwa sababu ya jina langu kuwa ni Muhammad.’ Aliipata kutoka wapi ahadi hii na dhamana hii? Sisi twawajua watu wengi ambao ni madhalimu na wa-Komunisti walio miongoni mwa Waislamu wenye majina ya Muhammad. Jee huku kuwapa majina ya Muhammad watu ndio kuthibitisha kuwa ni haki kwao kuingia peponi? Haliyakuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia binti yake ambae ni kipenzi chake, Faatimah (رضي الله عنها): *“Niombe utakacho katika nilivyomiliki Mimi sina chochote kiwezacho kukulinda kutoka kwa Allaah.”*

Katika Mlango wa 10, Busairi ameandika:

لعل رحمة ربي حين يقسمها * * * تأتي على حسب العصيان في القسم

Pengine Rehma za Mola wangu zinapogawanywa. Zitagawanywa kwa makadirio kulingana na madhambi (ya mtu).

Hayo [yote] hayakuswihi na wala hayana ukweli wowote. Ikiwa Rehma za Allaah hugawanya kulingana na daraja za madhambi yafanywayo kama iliyoashiriwa na Busairi kwenye shairi hilo lililotanguliwa, basi matokeo yake itawabidi Waislamu waongeze madhambi yao (wakiwa waume/wake) mpaka wajipatie ziyada kutokamana na Rehma za Allaah. Hili ni jambo ambalo hapana Muislamu yoyote au mtu mwenye fahamu zake njema awezae kusema maneno hayo, kwa sababu hapana shaka yakwamba inakwenda kinyume na maneno ya Allaah: **‘Bila shaka rehma ya Allaah iko karibu sana na (wale waja wake) wanaofanya mema.’** (Surah Al-Araaf Ayah no: 56)
Na pia maneno yake: **Na rehma yangu inaweza kukienea kila kitu. Lakini nitawaandikia (kweli kweli kabisa) wale wanaojikinga na yale niliyowakataza, na wanaotoa Zaka na wanaoziamini Aya zetu.** (Surah Al-Araaf Ayah no: 156)

Ameandika katika Mlango wa 3:

وكيف تدعو إلى الدنيا ضرورة من * * * لولاه لم تخرج الدنيا من العدم

Mtu mtukufu kama huyu ana mahitaji gani katika dunia hii. Kwani lau kama si kwa ajili yake, basi ulimwengu huu haungeliumbwa.

Busairi asema: ‘Lau kama si kuwepo kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), ulimwengu huu haungeliumbwa?’ [yaani; Ulimwengu huu umeumbwa kwa ajili ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)]. Allaah amemthibitisha yakuwa ni mrongo akasema:
Sikuwaumba Majini na watu ila wapate kuniabudu. (Surah Ad-Dhariyat Ayah no 56.)
Hata Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliumbwa kutokana na sababu hiyo peke yake ya kumuabudu Allaah peke yake na kuilingania Dini hiyo. Amesema Allaah katika kumuamrisha Mtume (صلى الله عليه وسلم): **Na umuabudu Mola wako mpaka ikufikie hiyo yakini (nayo ni mauti).** (Surah Al-Hijr Ayah no: 99)

Katika Mlango wa 5, ameandika:

أقسمت بالقمر المنشق إن له * * * من قلبه نسبة مبرورة القسم

Mimi naapa kwa mwezi ulogawanyika, kwa ilichokibeba. Wenye mafungamano na moyo wake (katika kuonyesha) ukweli wa kiapo changu.

Mshairi, Busairi anakula kiapo kwa Mwezi, haliyakuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa hakika amesema: *“Yoyote mwenye kuapa kwa asiyekuwa Allaah atakuwa amekufuru au atakuwa amefanya kitendo cha ushirikina* [anashirikisha washirika pamoja na Allaah katika ‘Ibaadah].” Hii ni hadeeth iliyo swaheeh iliyopokewa na Imaam Ahmad katika Musnad yake.

Katika Mlango wa 3, ameandika:

لو ناسبتْ قدرَه آياتُه عِظَماً * * * أحيا اسمه حين يُدعى دَارِسَ الرِمَمِ

Lau kama miujiza yake ingelikuwa kadiri (inayolingana na) daraja yake, kwa utukufu, Basi jina lake lingelikuwa, pindi linapolinganiwa, na uwezo wa kuifufua mifupa iliyo oza ikawa hai tena.

Maana ya mistari hiyo miwili iliyotangulia ya mashairi ni ifuatayo: ‘Ikiwa miujiza ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) yalikadiriwa kwa uwiano kulingana na daraja yake ya ubora, basi waliokufa na miili yao kuoza watafufuka warudi tena kwenye uhai kwa kulikumbuka jina la Mtume (صلى الله عليه وسلم).’
Chembelecho, jambo hili halikuwahi kutokea. Kwahivyo [kulingana na Busairi] Allaah (سبحانه وتعالى) hakumpa Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) haki yake katika

miujiza. Ni kama kwamba Busairi anampinga Allaah (سبحانه وتعالى), kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى) hakumkubalia na kumpa haki hii Mtume (صلى الله عليه وسلم)!! Huu ni urongo na uzushi juu ya Allaah (سبحانه وتعالى), kwa sababu kwa hakika Allaah (سبحانه وتعالى) alimpa kila Mtume miujiza kwa kiasi chake. Kwa mfano, Allaah alimpa na kumja'alia 'Issa (عليه السلام) miujiza ya kuwaponya vipofu, wenye mbalanga na kuwahuisha waliokufa [kwa amri ya Allaah], na Yeye Allaah (سبحانه وتعالى) vilevile akampa na kumja'alia kiongozi wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم) kwa kumpa miujiza ya Qur'an Takatifu, akaweza kuongeza chakula kichache na maji aliyokuwa nayo, na kugawanyika kwa mwezi vipande viwili n.k [*na kadhaalika*]

Kwa kumalizia, jambo la kushangaza ni kwamba baadhi ya watu wanaamini yakwamba mashairi haya yamejulikana kwa jina la 'Shairi la Busairi' na 'Shairi la Pozo' kwa sababu mshairi mwenyewe Busairi - kama wanavyodai - alikuwa mgonjwa, kisha akamuona (صلى الله عليه وسلم) ambaye aliyempa Busairi shuka la kujifunika refu lililokuwa wazi kwenye sehemu yake ya mbele na mikono mipana [kama kilemba]. Busairi akalivaa shuka hilo na akapoa ugonjwa wake. Kwa hakika huu ni urongo na uzushi kutoka kwa watu hawa kwa makusudio ya kuinua significance na umuhimu wa mashairi haya. Ataridhika vipi (صلى الله عليه وسلم) na sampuli hii ya maneno yenye kugongana na kupingana na Qur'an, uongofu wa (صلى الله عليه وسلم) na yenye ushirikina ulio wazi kabisa?

Inajulikana yakwamba mtu mmoja alikuja kwa (صلى الله عليه وسلم) akamwambia: "Apendavyo Allaah na upendavyo wewe," kwahiyo, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu kwa kumwambia: "*Umenifanya mimi kuwa ni mshirika wa Allaah! Sema apendavyo Allaah Peke yake."* Hadeeth hii imepokewa na Imaam an-Nasaa'I katika Sunan yake kwa silsila nzuri ya riwaya. Na neno la kiarabu "an-Nid" lina maana ya sawa [al-Mithl] au mshirika [ash-Shareek]. Kwahivyo, tahadhari Ewe ndugu yangu na Dada yangu katika Uislamu! Kutokamana na kusoma Shairi hili la Busairi na kila chenye kufanana na shairi hilo lenye kupingana na kwenda kinyume na Qur'an (na) uongofu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Jambo la kushangaza katika baadhi ya Miji ya Waislamu ni kwamba baadhi ya watu husoma mashairi haya pindi wakiwaaga wenzao wanaokufa au wanapowachukuwa kwenye maziara ya makaburi na kuongeza mambo mengine ya uzushi pamoja na uzushi huo wa upotofu. Ingawaje Mtume (صلى الله عليه وسلم) ameamrisha watu wawe kimya (wanyamaze) pindi wakifuata jeneza au wakenda kuzika.

MAZISHI *[Endelea kutoka Vol 21. Issue 3]*

IIbn Hazm amejibu hoja hii kwa kusema, "Kwa kila aliyezikwa katika wakati wa usiku, awapo ni yeye mwenyewe (صلى الله عليه وسلم), wakeze, au Maswahaba zake, basi ilikuwa ni kutokana na dharura iliyopatikana, kama vile kuhofia jua kali katika wakati wa mchana kwa wenye kuhudhuria - ambalo ni kali mno katika Mji wa al-Madeenah, au kuhofia mwili wa maiti usije ukaanza kuoza na kuvunda, au hata sababu nyengine ziwezazo kuruhusu mazishi ya usiku. Hafai mtu mwengine yoyote kuwadhania (hao waliozikwa nyakati hizo) (رضي الله عنهم) jambo lolote kwa ubaya." Lakini iwapo watu watalazimika kumzika mtu katika wakati wa usiku, wanaweza kutumia kandili na waiteremshe ndani ya kaburi ili walirahisishe jambo hilo la mazishi.. Amepokea Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimshusha mtu kwenye kaburi lake katika wakati wa usiku na ikawashwa kandili ndani ya kaburi."

UFAFANUZI KUHUSU KABURI: [UPANA, UREFU, NA UZURI]

Kaburi linatakiwa kuchimbwa refu na pana, na pambizo za miraba zenye kuta zilizo nyoroka na kushikana madhubuti.

Hisham Bin 'Aamir (رضي الله عنه) amepokea yakwamba katika siku ya Uhud, Waislamu wengi waliuliwa, na wakaumizwa wengi. Kwahivyo, Maswahaba wakasema: "Yaa Rasoolullaah! Kumchimbia kila maiti mmoja kaburi lake ni kazi nzito kwetu, sasa watuamrisha tufanyeje?" Akawajibu Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kusema: *"Chimbeni (makaburi), na muyapanue, yawe marefu na mazuri. Wazikeni wawili au watatu katika kila kaburi moja, na mumtangulize atakaekuwa na 'ilmu ya Qur'an zaidi."* Akaongezea Hishaam, "Babangu alikuwa ni wa tatu miongoni mwa watu watatu (ndani ya kaburi moja), lakini alikuwa akiijua Qur'an zaidi kuliko hao wawili wengine, kwahiyo yeye akawekwa mbele yao." Mtu mmoja miongoni mwa ma-Answaar alihadithia yakwamba alipokuwa ni kijana mdogo, alikwenda na babake na watu wengine pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye mazishi ya mtu mmoja katika ma-Answaar. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaketi karibu na pambizo ya kaburi na akamuamrisha mchimbaji: *"Lipanue (kaburi) kwenye upande wa kichwa, na ulipanue kwenye upande wa miguu. Kwa hakika, huwenda akapata mtende peponi."*

SHIMO - *LAHD*: Inaruhusiwa kuchimba kaburi liwe kama mfano wa shimo refu mstatili (rectangular) lililonyoka kiasi cha kwamba pande mbili fupi za mstatili ziwe zimeelekea upande wa Qiblah. Imependekezwa kuongezea hapo *lahd*, ambalo ni shimo jengine, lenye bukubwa kiasi cha kuingia mwili, lichimbwe karibu na sehemu ya chini ya kaburi ndani ya ukuta ulio kwenye muelekeo wa Qiblah. Baada ya mwili kulazwa ndani ya *Lahd*, huekewa mawe mazito nyuma yake. Malengo ya kuwekwa *Lahd* ni kwamba, utakapofukiwa ule mchanga kwenye kaburi hautokuwa ukimuangukia juu ya mwili wake na badala yake utakuwa ukianguka nyuma yake. Sampuli zote mbili za makaburi zilitumika katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم), lakini *Lahd* imependekezwa kutokamana na riwaya zifuatazo: Amepokea Anas Bin Maalik (رضي الله عنه): "Alipokufa Mtume (صلى الله عليه وسلم), palikuwa na wachimbaji makaburi wawili katika Mji wa al-Madeenah, mmoja wao alikuwa akichimba *Lahd* na mwengine alikuwa akichimba mashimo makubwa. Maswahaba wakasema, "Hebu tumuombeni Mola wetu atuchagulie, kisha tuwaite wote hao wawili. Atakaefika mwanzo ndiye atakaechimba kaburi hilo.." wakafanya hivyo, kisha mwenye kuchimba *Lahd* akaja mwanzo. Kwahivyo, wakamchimbia Mtume (صلى الله عليه وسلم) *Lahd*." Akapokea Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه): "Al-'Abbaas, 'Ali na al-Fadhl, waliingia ndani ya kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika kumzika. *Lahd* yake ilichimbwa na mtu wa ki-Answaar, ambaye ni yuleyule aliyechimba *Lahd* za *ma-Shaheed* wa *Badr*." 'Aamir, mwanae Sa'd Bin Abee Waqqaas (رضي الله عنه), alihadithia yakwamba babake aliamuru: "Nitengezeeni *Lahd* yangu, na munijengee mawe nyuma yangu - kama alivyofanyiwa Mtume (صلى الله عليه وسلم)." Imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas na Jareer (رضي الله عنهما) yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Lahd* ni zetu sisi (Waislamu), na mashimo wazi ni ya watu wengine." Amesema an-Nawawee (رحمه الله): "Hakuna maafikiano miongoni mwa wanavyuoni yakwamba kuzikwa ndani ya *Lahd* au kaburi lisilokuwa na lahd zote mbili zimeruhusiwa. Iwapo ardhi ni ngumu kiasi cha kwamba mchanga wake hautoporomoka, basi Lahd imependekezwa. Na iwapo ardhi itakuwa ni laini na mchanga wake unaweza kuporomoka, basi kaburi la shimo tu linafaa."